Toleo 43

# Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote

## USIWE NA MIUNGU MINGINE ILA MIMI

Wanadamu waliumbwa wakiwa na nafsi iliyo hai. Tangu kuumbwa kwa ulimwengu watu wamekuwa na shauku ndani yao ya kuwa wakiabudu kitu. Hata ingawa Yehova alitaka awe ndiwe anaabudiwa na wanadamu, na ingawa Yeye pekee ndiye anaweza kutosheleza haja hizo kubwa za kiroho zilizopo ndani ya wanadamu, wanadamu waliunda miungu ya uongo, na wakajitoa ili kutumikia sanamu zinazoweza kuguzwa, na zile sisizoweza kuguzwa, pamoja na falsafa tofauti tofauti. Hii ndiyo ibada ya sanamu, mtu kuabudu au kutukuza mifano, miungu ya uongo, au kitu kingine chochote ambacho kimechukua mahali pake Mungu. Kitu chochote cha maumbile au cha kiroho ambacho sio Mungu, na ambacho mioyo ya wanadamu inakitukuza, kinachochukua wakati wao, nguvu zao, pesa zao, na kujitoa kwao, ni ibada ya sanamu.

Kumekuwa na sanamu na miungu ya aina tofauti ambayo imejulikana kwa majina mengi kwa maelfu ya miaka katika enzi inayojulikana kama ya mapambazuko. Agano la Kale wakati mwingi imenena kuhusu miungu ya uongo na sanamu za mapagani. Dagoni, ambaye alikuwa na kichwa cha binadamu na mwili wa samaki, alikuwa mungu wa Wafilisti (1 Samueli 5:1-5). Merodaki au Beli, wa Yeremia 50:2 alikuwa "bwana wa miungu ya mbingu na nchi" wa watu wa Babeli. Naye Baali, mungu wa jua, alikuwa ndiye mungu mkuu wa watu wa Kanaani.Wafalme 18 inasema kuhusu makabiliano kati ya Eliya na manabii wa Baali, huku wakiomba moto kushuka toka mbingu. Na katika 1 Wafalme 11:33 tunasoma kuhusu Ashtorethi, mungu wa kike wa uwezo wa uzazi wa Wasidoni; na kuhusu Kemoshi, mungu wa Wamoabi; na Milkomu, mungu wa uaguzi wa Waamoni. Naye Moleki, mungu wa moto ambaye watoto walitolewa kafara kwake ametajwa katika Walawi 18:21. Hawa ni baadhi ya miungu wa kuundwa, viumbe vya kifumbo ambavyo vimeelezewa kwa sifa za kibinadamu na wanyama, na ambavyo vilitengenezwa kutokana na mawazo ya wanadamu.

Maandiko yametoa maelezo kuhusu ukosefu wa msimamo dhabiti wa wana wa Israeli katika vizazi vyote wakati walipokuwa wakimtumikia Mungu, wakawa wanageuka na kuabudu sanamu za nchi hiyo. Hapo Mlima Sinai Waisraeli walimuagiza Aaroni awatengenezee ndama wa dhahabu kwa kuiga mifano ya Wamisri, ambao waliabudu sanamu zilizoundwa kwa njia ya kuyeyusha (Kutoka 32:1-4). Naye Musa akashuka kutoka mlimani akiwa na amri ya Mungu, "Usiwe na miungu mingine ila mimi. Usijifanyie sanamu ya kuchonga . . . Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, BWANA, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu" (Kutoka 20:3-5). Amri hii ya Mungu ni ya kimsingi, na inawahusisha watu wote, kwamba "hutamwabudu mungu mwingine" (Kutoka 34:14). Yesu naye akasisitiza amri hii katika Agano Jipya: "Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake" (Luka 4:8).

Aina zote za ibada za sanamu ni dhambi, isipokuwa tu ibada iliyotolewa kwa Mungu wa Mbinguni. Walawi 26:1 inaonya watu kutotengeneza sanamu, na mifano ya kuchongwa, na kwamba watu wasiabudu sanamu kama hizo. Kumbukumbu 4:15-19 imeonya watu wasiharibu nafsi zao kwa njia ya sanamu.

*(Endelea katika Ukurasa 2)*



"Usiwe na miungu mingine ila mimi . . . kwa kuwa mimi, BWANA, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu."


| Tahariri | Mafunzo ya Biblia: Ibada za sanamu | Nakala Andamizi: Ibada za Sanamu Ulimwenguni | Mifano, Picha Takatifu, Miungu, na Mazoea | Je, Wajua? Neno Linalofaa kwa Msimu Huu |
|---|---|---|---|---|
| 3 | 4 | 5-6 | 7 | 8 |

# MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

**Neno la Mungu**
2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

**Uhusiano wa Upendo**
Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

**Toba**
Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

**Uzao Mpya**
Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6

**Uhuru Kutokana na Dhambi**
1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

**Ujazo wa Roho Mtakatifu**
Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

**Utakatifu**
Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16, Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

**Ufalme wa Mungu**
Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

**Kanisa**
Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13, Kol. 1:18

**Umoja**
Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

**Kanuni za Kanisa**
Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27, Yn. 13:14-17

**Uponyaji wa Kiungu**
Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

**Utakatifu wa Ndoa**
Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3, I Kor. 7:10-11

**Urembo wa Nje**
I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

**Mwisho wa Nyakati**
2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt. 25:31-46

**Kupenda Amani**
Lk. 6:27-29, 18:20

**Ibada**
Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

**Wajibu Mkuu**
Mk. 16:15

*(Inaendelea kutoka Ukurasa 1)*

Wakaonywa dhidi ya kutengeneza sanamu zenye mfano wa wanyama au wanadamu. Pia wakaonywa dhidi ya kuabudu jua, mwezi, wala nyota.

Mungu wa kweli ni mmoja, na heshima, sifa, utukufu na ibada zinahitaji kutolewa kwake peke yake. Yesu alitanguliza amri yake ya upendo kwa kusema ukweli wa kimsingi: "Sikia, Israeli, Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja" (Marko 12:29). "Zaidi yangu mimi hapana Mungu" (Isaya 44:6). Miungu mingine yote inahitaji kuharamishwa, kwa maana ibada zinazotolewa kwa sanamu za wanadamu humnyima Mungu ibada ambazo zinastahili kutolewa kwa jina lake peke yake.



Katikati ya sanamu na michoro ya kiungu iliyokuwako katika Mlima wa Marisi, mtume Paulo alitoa hotuba ya ajabu kuhusu Mungu wa kweli, ambaye ni muumba wa mbingu na nchi (Matendo 17:22-31). Mungu haishi katika hekalu ambazo zimeundwa kwa mikono ya wanadamu, na Yeye haabudiwi kwa mikono kama hiyo. Yeye ndiye anayetoa uhai na pumzi, na Yeye ndiye atakayehukumu ulimwengu katika siku ambayo amechagua. Mungu huyu hatengenezwi kwa dhahabu, fedha, au mawe; na pia Yeye hapatikani katika michoro au maumbile mengine ya kibinadamu. Yeye ndiye muumbaji wa ulimwengu. Na anaye mwana, Yesu, ambaye alisulubiwa na kufufuliwa tena kutoka kwa wafu baada ya siku tatu. Ni Mungu HUYU pekee ndiye anaweza kuletea nafsi ya mwanadamu amani, na pia kutosheleza shauku za ndani za nafsi ya binadamu. Kwa kweli Mungu astahili sifa zetu, kwa maana vitu vyote viliumbwa ili kumpendeza (Ufunuo 4:10-11).

> "Hatutakiwi kuwa na miungu mingine iliyotengenezwa, au iwe ndani ya mioyo yetu."

Basi mifano yote inayoabudiwa, sanamu zote zinazofanyiwa ibada, na vitu vyote vinavyotukuzwa na wanadamu vinahitaji kutupiliwa mbali sana na maisha yetu. Mungu ni Mungu wa wivu (Kutoka 34:14), na hatokubali tuchanganye ibada kwake na ibada kwa sanamu. Kuna mifano mingi na miungu mingi isiyo ya kweli, ambayo watu husali kwake hata katika siku hizi zetu. Sanamu hizi zaweza kujulikana kwa majina tofauti, ikilinganishwa na yale ya kale, lakini kwa kweli zingali ni miungu na sanamu za uongo. Nchi nyingi, makabila, na mataifa, wangali wanaendelea kujiingiza katika ibada za sanamu. Hii kwa kweli ni kujitumbukiza dhambini.

Hatutakiwi kuwa na miungu mingine iliyotengenezwa, au iwe ndani ya mioyo yetu. Hata ingawa baadhi ya watu wamezikataa sanamu, ukweli ni kwamba, hata Wakristo wengi wamejihusisha na kufungwa na ibada za kipagani na pia miungu ya uongo ya hapo siku za kale. Hebu basi tuyatakase maisha yetu, na ibada zetu tuzitoe kwake Mungu pekee, na kumpendeza tu yule Mungu mmoja wa kweli. ■

Gazeti la *Ukweli wa Injili* ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwahimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tutembelee katika tovuti yetu ya *www.thegospeltruth.org* na ujiandikishe ili uwe ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tayari ili uweze kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika nchi nyingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kupitia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako.

—Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@the gospeltruth.org

# Tahariri



*Mimi ni BWANA; ndilo jina langu; na utukufu wangu sitampa mwingine, wala sitawapa sanamu sifa zangu.* —Isaya 42:8

Mungu ni mwenye utukufu na kazi zake ni za ajabu. Hakuna kitu chochote mbinguni au nchini ambacho kifananishwa hata kidogo na utukufu na nguvu zake Bwana Mungu. Yeye anastahili heshima na utukufu, na kamwe hawezi kutoa sifa hizo zake na utukufu kwa kiumbe kingine chochote au kwa sanamu za kutengenezwa. Mungu pekee ndiye anaweza kuwakomboa wanadamu, na Yeye pekee ndiye anayeweza kutoa kipawa cha uzima wa milele.

Somo la robo hii ya mwaka ni kuhusu ibada ya sanamu. Ulimwengu una dini nyingi ambazo watu wanasujudu na kutoa ibada kwa sanamu. Kuna watu wengi ambao wanaabudu sanamu ambazo hazikuchongwa kutokana na mawe au kuundwa na mafundi wa vitu vya fedha. Watu wanajitoa ili kuabudu vitu vya ulimwengu, na hata ingawa wanadamu wengi hawawezi kukubali ukweli huu, hii pia ni ibada ya sanamu.

*Tutembelee www.thegospeltruth.org ili kujiandikisha na kupata jarida za mbele.*

Watu wa Kipagani na wenye kufanya ibada ambazo sio za kweli wanahitaji kukataa miungu yao ya uongo na kumfuata Mungu mmoja wa kweli. Wanahitaji kuondoa nje ya manyumba yao picha hizo takatifu na mifano hiyo ya sanamu, na Neno la Mungu lifanyike kuwa ni nambari moja mioyoni mwao. Wakristo wengi wanaweza kukubali hayo, lakini tuseme nini kuhusu miungu mingine? Je, tuseme nini kuhusu mungu wa mali, na mungu wa utaifa? Je, tuseme nini kuhusu mungu wa nafsi ya mtu? Na je, tuseme nini kuhusu sanamu ya mafundisho ya kikanisa, na sanamu ya wachungaji na manabii? Je, sisi kama Wakristo tunaweza kutambua kwamba mambo hayo pia ni matendo ya ibada ya sanamu?

Na je, tuseme nini kuhusu vile tunatumia wakati wetu? Huenda ikawa kwamba mitandao ya kijamii au michezo ni sanamu zetu? Kwa kweli hizi ni sanamu ikiwa tunaziruhusu kuongoza vile tunatumia wakati wetu, na tukiziruhusu kutawala maisha yetu. Ikiwa tumejitolea kwa mambo hayo zaidi ya vile tunamwabudu Mungu, je, si hii ni ibada ya sanamu? Ni jambo la kushangaza kwamba watu waweza kutumia pesa zao na wakati wao kwa mambo ya ulimwengu huu bila kujali, lakini ikifika wakati wa kumtumikia Bwana, wanasema kwamba hawana pesa wala wakati wa kutosha. Je, si jambo hili linastahili kutusumbua rohoni?

Tunahitaji kujichunguza kibinafsi na kuwa wakweli kabisa ili tuweze kukubali kwamba huenda kuna mambo maishani mwetu ambayo tumejitolea kwayo kwa njia ambayo inamnyima Mungu utukufu na cheo ambacho ni Yeye pekee anastahili kuwa nacho. Sisi hutazama mambo kwa njia ya kifupi na ya ubinafsi wa kimwili. Basi hebu basi Bwana atusaidia kurudi hatua moja nyuma na kutazama maisha yetu na matendo yetu huku tukijiuliza swali: "Je, Mungu anaona jambo hili vipi?" Ni ujumbe gani sisi huwa tunampatia Muumbaji wetu wakati tumejiingiza katika mazoea ya ibada za sanamu, au tunajihusisha na vikundi vya watu kwenye tamasha za kujifurahisha, huku daima tukidai na kusema kwamba, "Moyo wangu u sawa tu."

Ndoa zetu, kama ilivyo kweli na uhusiano wetu na Mungu, zinahitaji kuwa ni uhusiano wa mtu mmoja pekee na mwenzake, wakiwa peke yao. Je, ni ujumbe gani nitakaokuwa namtumia mke wangu ikiwa katika dawati langu nimeweka picha ya msichana kipenzi changu wa hapo mbeleni, na kusherehekea siku yake ya kuzaliwa mwaka baada ya mwingine? Je, mke wangu ataelewa ikiwa nitamwambia kwamba jambo hili kamwe silitilii maanani moyoni mwangu? Je, si jambo hilo pia ni la kweli kwa uhusiano wetu na Mungu? Bwana, twaomba utusaidie kuondoa sanamu zote maishani mwetu ili tukupende wewe Mungu wetu kwa mioyo yetu yote.

Michael W. Smith

Januari, 2023

## Je, Mungu ni wa Kwanza Maishani Mwako? Tambua Sanamu za Kisasa

Je, ni mambo gani napenda?

Je, kutosheleka kwangu kunatokana na nini?

Je, ni mambo gani mimi huwazia sana?

Je, mimi hutumia wakati wangu mwingi wapi?

Je, mimi hutumia pesa zangu na nini?

| | |
|---|---|
| **Pesa/Mali** | **Sio ya Kiungu** |
| **Kazi/Cheo** | **Simu/Teknolojia** |
| **Ushawishi/Kujulikana** | **Mafundisho ya Kidini** |
| **Kupendeza Kimwili** | **Elimu** |
| **Michezo/Burudani** | **Utaifa** |
| **Mahusiano Ambayo** | |



# Mwongozo wa Kujifunza Biblia

## Somo: Kuabudu Sanamu

**Somo la Maandiko:** *Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake.* —Luka 4:8

**Maana:** Maana ya ibada ya sanamu ni "kuabudu sanamu, mifano, au kitu chochote ambacho sio Mungu; ni kuabudu miungu ya uongo. Kupenda kitu sana, kukitukuza kitu kingine; kuheshimu au kupenda kitu mpaka unakitukuza" (*Kamusi ya Merriam-Webster*).

**Muhstasari:** Kutukuza au kuabudu kitu chochote ambacho si Mungu ni kuabudu sanamu — iwe ni sanamu ya kweli, mungu wa kujiundia, dini za kibinadamu, au kitu kingine chote cha ulimwengu huu ambacho ndicho unapenda sana, kinachochukua wakati wako, nguvu, au mali yako.

### I. Kuna Mungu Mmoja Tu

A. Marko 12:28-29 Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja.
B. Isaya 44:6 Zaidi yangu mimi hapana Mungu.
C. 1 Timotheo 2:5 Mungu mmoja na mpatanishi mmoja.
D. Ufunuo 4:10-11 Bwana astahili sifa.

### II. Ibada za Sanamu Zinaharamishwa

A. Kutoka 20:3-5 Msiwe na miungu wengine . . . Bwana ana wivu.
B. Kumbukumbu 4:15-19 Msiabudu sanamu, wala jua, mwezi, au nyota.
C. Walawi 26:1 Msitengeneze sanamu.
D. Kumbukumbu 7:3-4 Msioe wanaoabudu sanamu.

### III. Kumwabudu Mungu Peke Yake

A. Luka 4:7-8 Kumwabudu Yeye pekee.
B. Mathayo 6:24 Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili.

### IV. Mungu wa Kweli Akilinganishwa na Sanamu

A. Matendo 17:22-31 Mungu ni Muumbaji, hakuumbwa.
B. Kutoka 4:28 Kazi ya mikono ya watu.

### V. Ibada ya Sanamu Katika Agano la Kale

A. Ndama wa Dhahabu: Kuwakilisha Yahweh na vinyago vya Misri (Kutoka 32:1-4)
B. Sanamu ya Dhahabu ya Nebukadreza (Danieli 3:1-5).
C. Dagoni: Mungu wa Wafilisti; kichwa cha binadamu na mwili wa samaki (1 Samueli 5:1-5).
D. Merodaki (Marduki, Beli): Bwana wa miungu ya mbingu na nchi wa Kibabeli (Yeremia 50:2).
E. Baali: Mungu mkuu wa watu wa Kanaani (1 Wafalme 18:21-40).
F. Ashtorethi: Mungu wa Wasidoni wa kuzaa na wa uwezo wa uzazi.
G. Kemoshi: Mungu wa kitaifa wa Wamoabi.
H. Milkomu: Mungu wa uaguzi wa Waamoni (1 Wafalme 11:33).
I. Moleki: Mungu wa moto ambaye kwake watoto walitolewa kafara.

### VI. Mungu wa Dunia Hii

A. 2 Wakorintho 4:4 Mungu wa dunia hii hupofusha fikira za wanadamu.
B. Waefeso 2:2 Mfalme wa uwezo wa anga.
C. Waefeso 6:10-13 Mamlaka na wakuu wa giza.

### VII. Ibada za Dini za Uongo na Tamaduni

A. Ufunuo 14:8-10 Mnyama na sanamu yake.
B. Marko 7:6-8 Kutukuza tamaduni za wanadamu.

### VIII. Kuabudu Wanadamu

A. Matendo 12:21-23 Herode anatukuzwa kama mungu.
B. 2 Wathesalonike 2:3-4 Mtu wa kuasi.
C. Matendo 14:12-15 Paulo na Barnaba wakataa heshima.
D. Ufunuo 19:10 Usimwabudu mtumishi.
E. Yohana 7:16-18 Kutukuza nafsi yako ni kinyume na Kristo.
F. 2 Wakorintho 4:5 Msijihubiri nyinyi wenyewe.

### IX. Ibada ya Sanamu Katika Agano Jipya

A. Wakolosai 3:5 Tamaa ni ibada ya sanamu.
B. Wafilipi 3:19 Mungu wao ni tumbo.
C. Warumi 16:18 Kujali maslahi yako binafsi badala ya yale ya Yesu.

### X. Kuabudu Mambo yaa Dunia

A. 1 Yohana 2:15-16 Msipende mambo ya dunia.
B. Warumi 1:23-27 Maumbile; ushoga.
C. 1 Timotheo 2:3-4 Kupenda fedha.
D. 2 Timotheo 2:3-4 Shughuli za dunia.

### XI. Hukumu Juu ya Ibada za Sanamu

A. Wagalatia 5:19-21 Waabudu sanamu hawataurithi ufalme wa Mungu.

Tamati

*Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili; kwa maana atamchukia huyu, na kumpenda huyu; ama atashikamana na huyu, na kumdharau huyu. Hamwezi kumtumikia Mungu na mali.*
*—Mathayo 6:24*

# IBADA ZA

## SANAMU ULIMWENGUNI

Sio lazima mtu aangalie nyuma katika siku za ustarabu wa kale ili akutane na ibada za sanamu na miungu wa uongo. Miungu hii ya sanamu imetuzunguka kote katika jamii za kisasa. Ibada ya sanamu inamaanisha zaidi ya mtu kusujudu mbele ya sanamu ya kuchongwa kama ishara ya kuabudu; bali ni kitu chochote kile ambacho mtu amekipenda na kujitoa kwake zaidi yake Mungu. John Calvin alisema ukweli alipoandika na kusema: "Daima moyo wa mwanadamu ni kiwanda cha kutengeneza sanamu."



"Wakati kitu kimepewa umuhimu zaidi ya Mungu na Neno lake na kitu hicho kinaaminiwa kwamba kitaleta hali ya kutosheleka, basi hiyo ni sanamu."

### Ibada za Sanamu Katika Siku Zetu

Kinyume na sheria yake Mungu, kuna dini nyingi za kisasa ambazo watu husujudu mbele ya sanamu zilizotengenezwa kwa chuma au mawe. Hata hivyo, hata ingawa jamii nyingi ulimwenguni zimekataa sanamu hizo, kuna sanamu zingine kubwa na zenye nguvu zaidi ambazo ziko katika mioyo na fikira za wanadamu, na ambazo kwake watu wanatumia wakati wao, pesa zao, na hata kuwa na upendo nazo mioyoni mwao. Kitu chochote ambacho tumekitukuza zaidi yake Mungu na kukifanya kuwa ndicho tunakuwa makini sana kwake na kukipatia kipa umbele maishani mwetu, basi hicho pia ni sanamu. Ibada ya sanamu hufanyika moyoni, na huwa ni kwa kile ambacho mtu anakipenda, anakiamini, na anakiabudu.

### Vita vya Kiroho

Sisi tu vitani dhidi ya Shetani na dhidi ya maroho yake hadaa, ambayo inafanya jitihada kuondoa mioyo yetu kutoka kwa ibada ya kweli ya Mungu. "Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho" (Waefeso 6:12). Nguvu za uovu zimetuzunguka, na zinawaongoza watu kuabudu katika madhabahu ya kibinafsi, ya burudani, michezo, dini, siasa, utaifa, sayansi, elimu, na ya kupenda mali ya dunia. "Mungu wa dunia hii amepofusha fikira zao wasioamini" (2 Wakorintho 4:4).

### Ibada ya Sanamu Katika Dini

Ibada ya sanamu haiko tu katika upagani, bali pia katika madhehebu ya Ukatoliki na ya Kiprotestanti. Kanisa Katoliki limejaa mazoea ya kipagani na tamaduni ambazo hazina msingi wake katika Neno safi la Mungu. Kutukuzwa kwa taasisi yoyote ya kidini ni ibada ya sanamu. "Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za Mwana-Kondoo" (Ufunuo 14:9-10). Mara nyingi watu hujitoa mhanga kufaidi ushirika wao au kikundi chao cha kidini, zaidi ya maslahi yake Kristo (Mwenyewe). Hii ni ibada ya sanamu. Katika Marko 7:6-9 Yesu alinena kuhusu watu ambao walimtukuza kwa midomo yao, huku mioyo yao ikiwa mbali naye. "Ninyi mwaiacha amri ya Mungu, na kuyashika mapokeo ya wanadamu." Hata ingawa watu wanaweza kudai kwamba wanampenda Mungu, ni ibada ya sanamu kama watatukuza tamaduni zao za kidini zaidi ya urahisi wa Neno la Mungu. Jambo hili laweza kuwa la kweli hata kwa waumini wa Kanisa la Mungu. Kuwa mwaminifu na mtu kujitolea kwa tamaduni au mafundisho ya kidini (hata kama ni jambo nzuri) laweza kuwa ni ibada ya sanamu kama jambo hilo litapewa umuhimu mkuu maishani mwa mtu au katika kusanyiko la Wakristo.

### Kuabudu Wanadamu

Kuwatukuza viongozi wa kisiasa na kidini na kuwapa uwezo wa maisha yako na kuwaabudu kwa njia ambao Mungu pekee anastahili ni ibada ya sanamu. Katika Matendo 12:21-23 Herode aliwapatia watu hotuba kemkem. Ndipo wakapaza sauti na kusema, "Ni sauti ya Mungu, si sauti ya mwanadamu." Malaika wa Mungu akampiga, akaliwa na chango, kwa sababu "hakumpa Mungu utukufu." Wathesalonike wa pili 2:3-4 inatuonya dhidi ya kudanganywa, kwa maana mtu wa kuasi atajitukuza zaidi ya Mungu na atataka kuabudiwa kama Mungu. Mara nyingi andiko hili huhusishwa na papa wa Ukatoliki ambaye amejitangaza kuwa ndiye amesimama mahali pake Kristo humu duniani. Msimamo huu ni wa kukufuru na ni ibada ya sanamu. Lakini pia kuna "mapapa wengine wengi wadogo" ambao hujulikana kama wasimamizi, wachungaji, na viongozi wa makusanyiko na vikundi vya kikanisa. Wao hujiweka mahali palipotukuka, na maneno yao huchukuliwa kwamba yana umuhimu kwa kiwango cha Maandiko. Watu wanaweza kuwashangaa na kusema kwamba viongozi hao wao wa kidini ni watumishi wa Mungu, lakini hii ni ibada ya sanamu. Kristo peke yake ndiye anastahili sifa, sio mwanadamu. Paulo na Barnaba walifanya

*(Endelea katika Ukurasa 6)*

(Inaendelea kutoka Ukurasa 5)

miujiza ambayo ilifanya watu kuanza kuwatukuza kama miungu ambao walikuja katikati ya wanadamu (Matendo 14:12-15). Lakini watumishi hawa wa kweli wa Mungu walikataa sifa hizo na kutukuzwa huko, na kutangaza kwamba wao walikuwa "wanadamu hali moja na ninyi." Naye Yohana wa kitabu cha Ufunuo alipiga magoti ili kumwabudu malaika ambaye alikuwa amempatia maono. Lakini malaika akamwambia: "Angalia, usifanye hivi; mimi ni mjoli wako na wa ndugu zako walio na ushuhuda wa Yesu. Msujudie Mungu" (Ufunuo 19:10). Watu wote ambao wanaabudu viongozi wao wa kiroho ni waabudu sanamu, na hata wahudumu wa Injili ambao wanakubali aina hii ya sifa na kutukuzwa huko ni waabudu sanamu.



"Kujitukuza kwa aina yoyote kunaweza kuwa ni ibada ya sanamu. Ibada ya mtu kibinafsi ni aina moja ya ibada ya sanamu ambayo imesambaa sana katika kizazi hiki chetu."

## Kujiabudu Wewe Mwenyewe

Kujitukuza kwa aina yoyote kunaweza kuwa ni ibada ya sanamu. Ibada ya mtu kibinafsi ni aina moja ya ibada ya sanamu ambayo imesambaa sana katika kizazi hiki chetu. Hii inapatikana katika mambo ya kiroho na pia katika mambo ya ulimwengu. Yesu alisema, "Yeye anenaye kwa nafsi yake tu hutafuta utukufu wake mwenyewe" (Yohana 7:16-18). Katika vikundi vya kidini kuna wahudumu wengi wa Injili ambao hujiongelea wao wenyewe na kutukuza matendo yao wenyewe, ilhali mtume Paulo alitangaza kwamba: "Kwa maana hatujihubiri wenyewe, bali Kristo Yesu ya kuwa ni Bwana" (2 Wakorintho 4:5). Tunaishi katika kizazi ambacho watu wanaamini sana fikira zao wenyewe, maoni yao, na njia zao wenyewe. Wanajipenda wao wenyewe, na wanaishi maisha ya ubinafsi na ya kujijali maslahi yao. Jambo hili ni ibada ya sanamu, kama vile tu tendo la kusujudu mbele ya sanamu kwa ibada.

Wafilipi 3:19 inanena kuhusu watu ambao "mungu wao ni tumbo, utukufu wao u katika fedheha yao, waniao mambo ya duniani." Watu wanakataa mambo matakatifu ya Mungu na badala yake wanajitoa ili kupata raha zao wenyewe na kujitosheleza. Wao wanatawaliwa na "tumbo zao" na wanafanya mambo ambayo yanafurahisha miili yao. Wao "hawamtumikii Bwana wetu Kristo, bali matumbo yao wenyewe" (Warumi 16:18). Jambo hili halihusiani tu na ulafi wa chakula tu, bali pia mambo yote ya kimwili ambayo huwatawala watu.

## Miungu wa Ulimwengu Huu

Mungu anastahili upendo wetu, lakini watu wengi wanatoa upendo wao kwa mambo ya ulimwengu huu. "Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia" (1 Yohana 2:15). Tamaa ya mwili, tamaa ya macho, na kiburi cha maisha zimekita mizizi kaika sanamu za kisasa. Je, watu wanatamani na kuabudu nini? Ni nini kinatawala wakati wako, pesa zako, na nguvu zako? Je, ni vitu gani watu wanatukuza na kutegemea wakati wao wa haja? Je, si raha za kimwili, utaifa, mavazi, michezo na burudani zinaenda sambamba na mambo haya yote? Mambo ambayo ni halali yanaweza kuwa ni sanamu. Watu wengi wanatoa dhabihu zao katika madhabahu ya sanamu hizi za kisasa.

## Kwanzia Ibada za Sanamu Hadi Kufikia Maisha ya Upotovu

Warumi 1:23-27 inasema kuhusu jinsi watu wamebadilisha utukufu wa Mungu na kufanya sanamu zenye mfano wa mwanadamu, ndege, na majitu. Mstari wa 25 unasema, "wakakisujudia kiumbe na kukiabudu badala ya Muumba." Jambo hili hufanyika kwa njia nyingi, lakini moja kwa moja andiko hili linahusika na tendo la kuabudu kiumbe, na linatumika kwa mambo ya tamaa na matendo ya ushoga. Hata ingawa ushoga ni mwingi katika jamii na hata umehalalishwa na watu wengine, ilhali wengine wakiondolea matendo hayo lawama, haya matendo kwa kweli ni dhambi, na ni kuabudu sanamu kwa kiwango cha hali ya juu sana.

## Kuabudu "Vitu"

Wakolosai 3:5 inatufunza kwamba kutamani ni ibada ya sanamu. Kupenda mali ya dunia, utajiri, kiburi, nguvu, na kutambuliwa na watu ni ibada ya sanamu, kwa sababu hii inaenda kinyume na lengo na sababu ya kimsingi ya kumwabudu na kumtumikia Mungu. "Maana shina moja la mabaya ya kila namna ni kupenda fedha" (1 Timotheo 6:10). Wengi wameacha imani walipoanza kufuata na kutumikia mambo ya ulimwengu huu zaidi ya vile wanavyompenda Mungu Mwenyewe. Ni nini kinatawala wakati wako, pesa zako, nguvu zako? Je, wewe ushaweka Mungu na kazi yake katika kiwango cha juu zaidi ya vitu vingine vyote? Je, wewe hutenga wakati ili kuhudhuria ibada pamoja na watakatifu wengine kwa uaminifu, au unatoa vijisababu vya kutohudhuria ushirika, huku ukijitoa kutumikia malengo mengine maishani mwako? Mioyo ya watu husomeka kutokana na maamuzi na chaguo za maisha yao. Ni nini kinachoongoza uamuzi wako maishani, mahali utakapoishi, nani utaoa, utafanya nini, na kule utakakoenda? Je, inawezekana kwamba sanamu fulani imechukua mahali pa Mungu maishani mwako?

## Kutukuza Malengo ya Kijamii

Mtume Paulo alitoa onyo kwa Timotheo, "Hakuna apigaye vita ajitiaye katika shughuli za dunia" (2 Timotheo 2:3-4). Kwa kweli kuna malengo halali na mambo ambayo yanaathiri jamii kwa sasa, na ambayo tunahitaji kuyashughulikia. Lakini ni muhimu sisi tusijitumbukize ndani mambo hayo. Mambo ya kisiasa, kimaadili, kitabaka, na ya kijamii yanaweza kumteka mtu sana hadi ikawa ndio yanayomtawala, na ndipo hapo yanakuwa sanamu. Basi wewe mtoto wa Mungu uwe mwangalifu usijihusishe sana na kile ambacho kinaonekana kuwa ni lengo nzuri la kijamii. Punde si punde lengo hilo litakuwa ni muhimu zaidi ya Mungu, na njia zake za upendo, msamaha, na kustahimili.

## Mwabudu Mungu Peke Yake


Sanamu za siku zetu zina hadaa nyingi sana, na pia ni hatari zaidi ya sanamu zinazoonekana na zilizotengenezwa kwa dhahabu au fedha. Kuna Mungu mmoja, na upendo na utumishi wetu kwake unastahili kuwa ni kwake Yeye peke yake. Hebu basi tujichunguze tujue kama kuna sanamu ambazo zinahitaji kuvunjiliwa mbali kutoka kwa maisha yetu. Hebu tuziondoe na kujitakasa dhidi ya sanamu za ulimwengu huu, kwa maana kusema kweli, waabudu sanamu na "watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu" (Wagalatia 5:19-21). ■

# Mifano, Picha Takatifu, Miungu, na Mazoea

## AMBAYO MISINGI YAKE NI IBADA YA SANAMU




**Hirizi:** Kifaa ambacho kinachukuliwa kuwa na nguvu za kidini au kimuujiza, ambacho kinaweza kukulinda, kukuponya, au kuwadhuru watu wengine (kama kijilasaba kidogo, ki yin-yang, kifaa kinachofanana na mguu wa sungura, bangili, fuwele).



**Bikira Maria:** Maria, mama yake Yesu, ambaye Wakatoliki walianza kumwomba hapo karne ya tatu.



**Budha:** "Yule Aliyezinduliwa" au "Mwenye Elimu Yote" kutoka Kusini mwa Bara Asia. Alizinduliwa katika karne ya tano. Hata ingawa hachukuliwa kuwa ni mungu, wafuasi wa Budha husujudu mbele ya sanamu yake kwa heshima huku wakijaribu kupata nguvu nzuri za kiroho kutoka kwake.



**Ganesha:** Huyu ni mmoja wa miungu wa Kihindi anayejulikana sana. Yeye ni bwana wa uwezo wa kufaulu na anayeondoa vizuizi.



**Kizazi Kipya:** Kila kitu ni kimoja. Huu ni mkusanyiko wa imani za kiroho ambazo zinatafuta upatanisho katika maumbile asili, na kutoka ndani yake mtu. Mungu ni kila kitu, na mwanadamu ni mungu. Akili za mwanadamu ndizo hufanya mambo kuwa halali. Kuna mazingaombwe mengi yanayohusika hapa.



**Kuwatukuza Mababu:** Katika tamaduni zingine mababu wanatukuzwa kama roho, na inaaminika kwamba wanaweza toa onyo, kulinda, na pia kuathiri maisha ya kila siku ya wanadamu. Wakati mwingine watu hufanya maombi kwao na hata kuwaachia chakula.



**Uganga:** Matumizi ya nguvu za kimuujiza au uchawi ili kutawala maisha ya watu na pia matukio.



**Unajimu:** Hii inahusisha matendo ya kukisia au kubahatisha, na ambayo hutabiri matukio kwa utazamaji wa sayari na nyota. Falaki.

## SIKUKUU

Hata ingawa kuna njia halali za kufurahia sikukuu za kitaifa, mtoto wa Mungu kamwe hastahili kusherehekea sikukuu hizi kwa kulingana na watu wa ulimwengu. "Mtendapo neno lo lote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu" —1 Wakorintho 10:31.



**Pasaka** (Tofauti na Jumapili ya kufufuka): Hii huchukuliwa kuwa ni sikukuu ambayo mwanzoni ilikuwa ya kipagani, na ilikuwa ya kusherehekea mungu wa majira ya kuchipuka na uwezo wa uzazi. Kulikuwa na ishara ya uwezo wa uzazi huko Misri ya kale, na hili ndilo lilikuwa chimbuko la Sungura wa kusherehekea Pasaka. Mayai nayo yalikuwa ishara ya uwezo wa uzazi na uhai, na tendo la kupaka mayai rangi lilianzia katika tamaduni hizo za kipagani.



**Halowini:** Mwanzoni hii ilikuwa ni sikukuu ya kipagani ya kusherehekea Samhaini. Ulikuwa ni mwanzo wa msimu wa baridi huko Celtic; ilikuwa ni wakati wa kuheshimu waliokufa, na wakati ambapo vitenganishi vya walio hai na waliokufa vilikuwa hafifu sana. Malenge yalitumiwa kufukuza maroho waovu. Katika karne ya nane Kanisa Katoliki lilijaribu kubadilishi hii sherehe ya Celtic na kuifanya kuwa Siku ya Watakatifu Wote.



**Krismasi:** Mwanzoni hii ilikuwa ni sikukuu ya kipagani ambapo kulisherehekewa mwisho wa msimu wa baridi na kuzaliwa tena kwa mungu wa jua. Kanisa la Ukatoliki wa Kirumi lilichukua sikukuu hii na kuibatiza ikawa ya "Kikristo" ili wapagani ambao walikuwa wamekubali Ukristo waweze kuendelea na sherehe hizo. Chimbuko la matumizi ya shada za maua na miti ya kijani kibichi ilitokana na tamaduni za kipagani.

JE, **WAJUA?**




Chimbuko la Miinuko: Historia ya minara ilianza maelfu ya miaka iliyopita huko Misri katika ibada za kipagani. Ilikuwa ishara ya nguvu za uzazi kwa ajili ya heshima ya mungu wa jua na nguvu za uzazi. Mifano mingi ya kipagani iliingizwa katika Kanisa Katoliki la Kirumi katika karne ya nne. Mnara ulitumiwa kama mahali palipoinuka pa kuweza kuona mambo yote, na pia kwa kusudi la kusikika kwa kengele ya kanisa, kufukuza roho waovu, na kama ishara ya kufika mbinguni. Minara hii ilifanyika kuwa sehemu ya usanifu wa majengo ya kikanisa, na pia ikawa ishara ya kuonyesha jengo fulani ni mahali pa ibada.

Neno Linalofaa kwa Msimu Huu

# UTUKUFU WOTE UNAYE YEYE

*Lakini, kueni katika neema, na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo. Utukufu una yeye sasa na hata milele.* —2 Petro 3:18



Sanamu na minara ya ukumbusho huundwa ili tuwakumbuke wale waliokuwako mbeleni ili kuwapa wanadamu changamoto; vyuo vikuu vya kufana navyo hujengwa ili kuendeleza elimu ya kibinadamu na kutukuza akili za mwanadamu; mijengo mikubwa ya gorofa nyingi ni ushahidi wa uwezo na ubunifu wa wanadamu; na maktaba zilizojengwa kwa mawe na zile za kijiditali huwa zimejaa falsafa za wanadamu. Lakini ewe mtoto wa Mungu, utafanya juhudi ili uweze kuishi kwa kanuni gani za ulimwengu? Ni nani utapatia heshima na utukufu maishani mwako?

Lengo na kusudi la watoto wa Mungu linastahili kuwa ni kumtukuza Yesu Kristo, ambaye ni Bwana Mwokozi na mtawala wa ulimwengu. Wakati watu wa ulimwengu wanajitukuza wao wenyewe kwa kile ambacho wamefanya na wanapanga kufanya, kujitukuza kwetu kunastahili kuwa katika Kristo peke yake.

Basi hebu tujitahidi kumjua na kumwelewa Kristo ili tuweze kukua katika neema zake za Kiungu kupitia athari na nguvu za Roho wake Mungu. Kwa kiwango ambacho tutampenda na kumtii Mungu, ndivyo ambavyo kujisalimu kwetu na kujitoa kwetu kwake kutakuwa kukubwa zaidi, na tutazidi kukua katika sifa za Kristo Mwenyewe. Kwa kufanya hivyo Kristo pekee ndiye atakayetukuzwa. Basi hebu kila lengo, kusudi, juhudi, ndoto na jitihada zetu chimbuko lake liwe ni Kristo, huku daima tukitafua utukufu wa yule ambaye ni mwokozi mmoja pekee wa ulimwengu.

Heshima, utukufu na sifa zote zinastahili kupewa Yesu Kristo, kwa maana Yeye ndiye Bwana wa mabwana, Mfalme wa wafalme, Alfa na Omega, mwanzo na mwisho, mwanzilishi na mkamilishi wa imani yetu. Nguvu zote na utawala ni zake, na Yeye anatawala juu ya miungu wote na roho za ulimwengu huu.

Kwa kweli tunaweza, tunastahili, na hatuna budi—bila kizuizi wala aibu—kuishi kwa kumtukuza Bwana Yesu, daima, hadi mwisho wa dahari, ambapo milele tutakuwa katika uwepo wa ajabu wa Mungu mkuu. Yeye anastahili sifa na kutukuzwa katika kila hali maishani mwetu. Basi Yeye apewe utukufu wakati wa majaribu, tukiwa motoni, tukiwa gizani, tukidondokwa na machozi, na hata tunapokabiliana na mauti. Sisi kumtukuza Mungu silo jambo la kustahimili, bali ni jambo la heshima kubwa kwetu. ■

Anwani

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

Utakatifu kwa Bwana